

## TAASISI YA BIBLIA NA UTUMISHI

SANGA SANGA MOROGORO NOVEMBA 14-18/2016

MADA: BIBLIA MSINGI WA UMISHENI

### UTANGULIZI

Katika Mada hii tutajifunza juu ya Umisheni katika nuru ya Biblia.

Anguko la Mwanadamu linaelezwa katika Neno la Mungu Mwanzo 3: 1ff

Anguko hili lilileta athari zifuatazo:

- Uhusiano kati ya Mungu na Mwanadamu kuharibika
- Uhusiano kati ya Mwanadamu na Mwanadamu mwenzake kuathirika
- Mazingira kuharibika na mwanadamu kula kwa jasho

Matokeo yaliyoonekana mara baada ya Anguko

- Kaini kumwua Habili
- Uovu wa mwanadamu ukawa chimbuko la gharika kuletwa juu ya uso wa dunia
- Kuchafuliwa kwa usemi wa mwanadamu ili wasisikilizane.

***Mpango Mahususi wa Mungu wa kurudisha uhusiano wake na Mwanadamu.***

Mpango unaanza katika Mwanzo 11:10, lakini tamko lake lilitolewa katika Mwanzo 3:15cf Gal 4:4-7, Kor 2:13-15

- Ulianza na Abram na mke wake Sarai
- Akafuata Isaka na Rebeka
- Akafuata Yakobo na wake zake Lea na Rahel
- Baada ya Yakobo ni wana kumi na wawili wa Yakobo. Katika hawa alichaguliwa Yuda. Angalia Mwa 49:8-12. Cf Ufu 5 :1ff
- Katika kabila ya Yuda, Daudi mwana wa Yese alichaguliwa. Rum 1:1-4, 2Samweli 7:1ff
- 

Kilele cha Mpango Mahususi wa Mungu kurudisha uhusiano wake na Mwanadamu ni kwa Njia ya Msalaba wa Yesu Kristo. Angalia ufafanuzi wa Mtume Paulo katika waraka wake kwa Warumi.

### ANGALIZO

Hatuwezi kuzungumza juu ya Umisheni nje ya Msalaba wa Kristo kama Njia pekee ya kurudisha uhusiano kati ya Mungu na Mwanadamu na kurudisha mahusiano sahihi kati ya mwanadamu na mwanadamu mwenzake. Aidha mwanadamu hawezi kuwa na mtazamo sahihi juu ya mazingira nje ya ukweli wa Biblia

*Nafasi ya Kanisa katika kazi ya Umisheni. Mfano wa Kanisa Antiokia. Mdo 13:1ff*

*Mambo yapi tunayoweza kujifunza kutokana na Kanisa hili?*

Nafasi ya Mchungaji ni ipi katika Kanisa la Antiokia kuhusiana na kazi ya Umisheni?

## **HITIMISHO**

Nje ya Neno la Mungu, hatuwezi kuwa na mtazamo sahihi juu ya umisheni. Inawezekana kuwa na mambo mazuri, lakini yasiyo dumu milele. Umisheni utakaongusa moyo wa Mungu ni ule utakaoendana na mpango mahususi wa kumkomboa mwanadamu katika dhambi zake.